# Nusu nusu?

## Maoni ya wananchi kuhusu upatikanaji wa maji safi







## 1. Utangulizi

Upatikanaji wa maji safi umeendelea kuwa changamoto kwa Watanzania; asilimia 46 ya wananchi wanataja upatikanaji wa maji kama changamoto mojawapo kuu inayoikabili nchi[1]. Changamoto hii pia imekuwa ikioneshwa kwenye Malengo ya Maendeleo ya Milenia ya Umoja wa Mataifa (MDGs) na ni sehemu ya maeneo yaliyopewa kipaumbele katika mpango wa Matokeo Makubwa Sasa (BRN). BRN ina lengo la kurejesha upatikanaji wa maji kwa Watanzania milioni 5.3 ambao kwa sasa wanakabiliwa na usumbufu wa kupata maji ya bomba. BRN pia inalenga kusambaza maji kwa Watanzania wapya milioni 7 katika kipindi cha miaka miwili (hadi 2015/2016)[2]. Lengo la MDG lilikuwa ni kubwa zaidi: lilitaka asilimia 74 ya wakazi wa vijijini wapate vyanzo vya maji ya kunywa vilivyoboreshwa ifikapo 2015[2].

Kutokana na malengo haya mawili, muda huu ni muhimu na unapaswa kutumika kuwasikiliza wananchi na kujifunza kuhusu uzoefu wao kwenye upatikanaji wa maji katika maeneo yao. Je, wananchi wanaona upatikanaji wa maji safi na salama kama changamoto? Ni muda gani unaotumika katika kutafuta maji kwa ajili ya mahitaji yao, na je, ni changamoto gani wanazokumbana nazo? Pengine cha muhimu zaidi ni kubaini kuwa, je, wananchi wameona tofauti yoyote kutokana na mipango mikubwa ya serikali kwenye sekta ya maji, hasa hasa kupitia mpango wa Matokeo Makubwa Sasa?

---

1 Sauti za Wananchi, Muhatasairi Na. 27, *Acha watu Waongee*, Septemba 2015

2 "Maelezo ya jumla kuhusu Maji-NKRA ." *Ofisi ya Rais ya Ufuatiliaji wa Miradi*. Tovuti ya N.P., n.d. http://www.pdb.go.tz/?q=node/40

3 "Ripoti ya nchi ya Tanzania kuhusu Malengo ya Maendeleo ya Milenia." Tovuti ya UNDP, 2011.

Muhtasari huu umeandikwa na umeandaliwa na Twaweza East Africa.
Umetolewa Novemba 2015

S.L.P 38342, Dar es Salaam, Tanzania.
Simu: +255 22 266 4301 | Barua Pepe: uwazi@twaweza.org | www.twaweza.org/sauti

Twaweza ni sisi

Dunia inahama kutoka Malengo ya Maendeleo ya Milenia na kwenda kwenye Malengo Mapya ya Maendeleo Endelevu. Tathmini ya uzoefu wa wananchi katika kupata maji safi na salama pia inatoa mtazamo wa jumla wa maendeleo yaliyofikiwa hadi sasa na inagundua kuwa maji yanaendelea kuwa kipaumbele muhimu katika malengo haya; wananchi wanaolengwa ni wengi zaidi: kila mtu anatakiwa kupata maji safi ifikapo mwaka 2030.

Takwimu kwenye muhtasari huu zimetokana na utafiti wa *Sauti za Wananchi* ambayo ni mpango mojawapo wa Twaweza. *Sauti za Wananchi* ni utafiti wenye uwakilishi wa kitaifa, unaofanyika mara kwa mara kupitia simu ya mkononi. Utafiti huu una uwakilishi wa Tanzania Bara tu. Taarifa juu ya mbinu za utafiti zinapatikana hapa www.twaweza.org/sauti. Takwimu za muhtasari huu zilikusanywa kutoka kwa wahojiwa 1,852 wa jopo la pili la wananchi waliopigiwa simu na *Sauti za Wananchi*. Matokeo ya muhtasari huu yanawakilisha awamu ya pili ya upigaji simu kwa jopo jipya la wahojiwa, iliyofanyika kati ya tarehe 9 na 26 Septemba 2015.

Matokeo muhimu:


- Ni wananchi wanne tu kati ya kumi wa vijijini ndio wanaopata maji safi ya kunywa kutoka vyanzo vilivyoboreshwa.
- Ni wananchi wasiozidi wanne kati ya kumi ndio wanapata maji ya bomba. Wengi huchota maji kutoka kwenye visima na madimbwi.
- Asilimia 57 ya wananchi huyatibu maji kwa matumizi ya nyumbani, na njia kuu wanayoitumia ni kuyachemsha.
- Uchotaji maji unachukua muda mwingi, na bado ni jukumu kuu la wanawake na wasichana.
- Maji machafu na umbali wa vyanzo vya maji ni miongoni mwa changamoto kubwa wanazokumbana nazo wananchi wa vijijini wakati wa kutafuta maji safi na salama. Changamoto kubwa kwa wananchi wa mijini ni gharama kubwa za maji na maji kutokuwa na uhakika wa kupatikana.
- Licha ya mpango wa *Matokeo Makubwa Sasa*, asilimia 80 ya wananchi hawaoni mabadiliko yoyote katika sekta ya maji.
- Ingawa imetangazwa sana, kipindupindu kimeenea sehemu ndogo tu nchini Tanzania.

# 2. Mambo saba kuhusu upatikanaji wa maji safi nchini Tanzania

## Jambo la 1: Wananchi wanne kati ya kumi wa vijijini wana chanzo cha maji safi ya kunywa kilichoboreshwa

Asilimia 41 ya wakazi wa vijijini wameripoti kuwa wanatumia chanzo cha maji safi ya kunywa kilichoboreshwa. Kwa mujibu wa Malengo ya Maendeleo ya Milenia, angalau asilimia 74 ya Watanzania vijijini wanapaswa kutumia chanzo kilichoboreshwa cha maji ya kunywa (mfano ni maji ya bomba, visima vilivyojengewa, na visima vya kufukuta) ifikapo mwaka 2015.

**Kielezo cha 1: Je, Tanzania imefikia Malengo ya Maendeleo ya Milenia kwenye maji?**





**Chanzo cha takwimu**: *Sauti za Wananchi* – Mohojiano ya Awali (Septemba 2015) na Ripoti ya nchi ya Tanzania kuhusu Malengo ya Maendeleo ya Milenia (2010)

## Jambo la 2: Wananchi wasiozidi wanne kati ya kumi wanapata maji ya bomba, ila walio vijijini wanahangaika zaidi

Upatikanaji wa maji ya bomba unaaminika kuwa na athari chanya juu ya usafi na afya[3], na unapunguza mzigo wa kuchota maji. Cha kusikitisha ni kwamba, ni asilimia 36 tu ya wananchi ndio wanaopata maji ya kunywa ya bomba. Takwimu hizi hazijabadilika tangu mwaka 2014[4]. Wananchi wengi wanategemea visima (asilimia 35) au maji ya kwenye madimbwi (asilimia 18), ambayo kwa ujumla siyo safi na salama.

**Kielelezo cha 2a: Chanzo kikuu cha maji ya kunywa kwenye familia yako ni kipi?**





**Chanzo cha takwimu**: *Sauti za Wananchi* - Mohojiano ya Awali (Septemba 2015)

Kukosekana kwa maji ya bomba ni tatizo kubwa zaidi katika maeneo ya vijijini. Wakati wananchi sita kati ya kumi (asilimia 58) wa mijini wanapata maji ya kunywa ya bomba (ama kwenye majengo yao au kutoka kwenye bomba lililo jirani na nyumbani), ni mwananchi mmoja tu kati ya wanne (asilimia 26) ya wananchi wa vijijini ndio anayepata maji ya bomba.

3 "Maji ya kunywa: Usawa, Usalama, na uendelevu." Tovuti ya UNICEF na Shirika la Afya duniani, 2011.

4 Muhtasari wa Sauti za Wananchi Na. 10, *Fedha Kibao, Maji kiduchu*, Aprili 2014

**Kielelezo cha 2b: Chanzo kikuu cha maji ya kunywa kwenye familia yako ni kipi?**





**Chanzo cha takwimu**: *Sauti za Wananchi* – Mohojiano ya Awali (Septemba 2015)

## Jambo la 3: Kuchemsha maji ndiyo mbinu inayotumiwa na wengi kutibu maji

Asilimia 57 ya wananchi wameripoti kuwa wanayatibu maji yao ili yawe salama kwa ajili ya kunywa. Wengi wao (asilimia 85) huyachemsha maji yao. Hata hivyo, idadi kubwa (asilimia 69) wameripoti kuwa wanachuja maji yao kabla ya kunywa, na baadhi (asilimia 38) huyaacha yatuwame uchafu uende chini. Hata hivyo, hizi siyo njia salama za kutibu maji kwa mujibu wa viwango[5] vya Shirika la Afya Duniani na UNICEF.

Walipoulizwa kwa nini hawatibu maji yao, wananchi watatu kati ya kumi walisema ni kutokana na kukosekana kwa muda na/au rasilimali (takwimu hazijaoneshwa kwenye kielezo).


**Kielelezo cha 3a: Unayatibu maji yako ili yawe salama kwa kunywa?**




**Chanzo cha takwimu**: *Sauti za Wananchi* – Mohojiano ya Awali (Septemba 2015)

5 "Maji ya kunywa: Usawa, Usalama, na uendelevu." Tovuti ya UNICEF na Shirika la Afya duniani, 2011

**Kielelezo cha 3b: Unayafanyia chochote maji yako ili yawe salama kwa kunywa?**





**Chanzo cha takwimu**: *Sauti za Wananchi* – Mohojiano ya Awali (Septemba 2015

## Jambo la 4: Asilimia 44 ya wananchi wanatumia zaidi ya nusu saa kuchota maji

Wakati idadi kubwa ya wahojiwa (asilimia 79) waliweza kupata maji ya kutosha ndani ya wiki mbili kabla ya ukusanyaji wa takwimu hizi (takwimu hazijaoneshwa), wananchi wanne kati ya kumi waliripoti kutumia zaidi ya dakika 30 kuchota maji kwa kila safari ya kufuata maji kwenye chanzo chao. Miongozo ya sera za serikali inapendekeza kuwa safari ya kwenda na kurudi kufuata maji kwenye chanzo haipaswi kuchukua zaidi ya dakika 30.

Mzigo wa kuchota maji haubebwi na wanafamilia kwa usawa. Kwenye kaya saba kati ya kumi, wanawake na wasichana ndio waliobeba mzigo mkubwa wa kuchota maji (takwimu hazijaoneshwa).

**Kielelezo cha 4: Inakuchukua muda gani kufika kwenye chanzo chako cha maji, kuchota maji na kurudi?**





**Chanzo cha takwimu**: *Sauti za Wananchi* – Mohojiano ya Awali (Septemba 2015)

## Jambo la 5: Zaidi ya wananachi sita kati ya kumi wanaona upatikanaji wa maji kama tatizo kubwa kwenye jamii zao

Licha ya kwamba wahojiwa wengi walikuwa na uwezo wa kupata maji waliyohitaji siku za karibuni, asilimia 65 bado wanaamini kuwa upatikanaji wa maji safi ya kunywa ni tatizo kubwa zaidi linalokaibili jamii yao (takwimu hazijaoneshwa).

Wananchi wengi bado wanakumbana na changamoto ya kupata maji, huku kukiwa na tofauti kubwa ya changamoto hizo katika maeneo ya vijijini na mijini. Wakazi wa vijijini walisisitiza kuwa changamoto yao kubwa ni umbali wa vyanzo vya maji (asilimia 47) na maji kuwa machafu (asilimia 40), wakati wakazi wa mijini walitatizwa zaidi na mgao wa maji (asilimia 43) na gharama kubwa ya maji (asilimia 40). Idadi inayolingana kwa wakazi wa mijini na vijijini waliripoti uhaba wa vyanzo vya maji kama changamoto kwao.

**Kielelezo cha 5: Ni changamoto zipi unazokumbana nazo katika kupata maji safi ya kunywa?**




**Chanzo cha takwimu**: *Sauti za Wananchi* – Mahojiano ya Awali (Septemba 2015)


## Jambo la 6: Licha ya jitihada za Matokeo Makubwa sasa, wananchi 8 kati ya 10 wanaona hakuna mabadiliko

Mpango wa Matokeo Makubwa Sasa (BRN) ulizinduliwa mwaka 2013, na uliweka mpango kabambe wa miaka miwili wa kuboresha sekta ya maji. Mpango huu ulilenga kutoa maji kwa Watanzania milioni saba ambao hawakuwa na huduma ya maji, na kuongeza idadi ya wakazi wa vijijini wanaopata maji kutoka asilimia 40 kufika hadi asilimia 67 mwaka 2015/2016. Hata hivyo, pamoja na mpango huu kufika mwaka wake wa pili, asilimia 80 ya wananchi hawajaona maboresho yoyote kwenye upatikanaji wa maji vijijini.

BRN inaripoti kuwa kumekuwa na ongezeko kubwa la upatikanaji wa maji lililotokea kati ya mwaka 2013/2014 na miaka ya nyuma. Mwaka 2013/2014, miradi ya maji chini ya BRN iliweka malengo ya kuongeza huduma ya maji kwa wananchi milioni 2.36. Kabla ya BRN,

wastani wa ongezeko la watu wanaopata maji safi na salama ilikuwa ni watu 300,000 hadi 500,000[6].

**Kielelezo cha 6: Mwaka 2013, Serikali ilizindua mpango mpya ujulikanao kama Matokeo Makubwa Sasa "BRN" na moja ya sekta katika mpango huu ni sekta ya maji. Je, umeona mabadiliko yoyote kwenye sekta ya maji katika jamii yako?**





**Chanzo cha takwimu**: *Sauti za Wananchi* – Mohojiano ya Awali (Septemba 2015)

## Jambo la 7: Kipindupindu hakijasambaa sana nchini Tanzania

Kipindupindu huenea kwenye mazingira machafu, na maji machafu yanaweza kubeba ugonjwa huu na kuwaambukiza watu pamoja na jamii zao. Hivi karibuni kumekuwa na taarifa nyingi kwenye vyombo vya habari za kuibuka na kuenea kwa kipindupindu nchini Tanzania. Licha ya taarifa za mara kwa mara kuhusu kipindupindu, ni asilimia 6 tu ya wananchi walioripoti kuwa wamemuona mgonjwa au wamesikia kuwa mtu fulani amepimwa na kubainika ana ugonjwa wa kipindupindu, ndani ya wiki nne kabla ya utafiti wetu.

**Kielelezo cha 7: Ndani ya wiki nne zilizopita, umewahi kumuona au kusikia ndugu, rafiki au jirani amegundulika kuwa kipindupindu?**




**Chanzo cha takwimu**: *Sauti za Wananchi* – Mohojiano ya Awali (Septemba 2015)

6 "Matokeo Makubwa Sasa! 2013/2014 Ripoti ya Mwaka." Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tovuti ya Ofisi ya Rais ya Ufuatiliaji wa miradi, n.d.

# 3. Hitimisho

Ni wazi kwamba upatikanaji wa maji safi na salama umeendelea kuwa changamoto kubwa kwa Watanzania. Serikali na washirika wa maendeleo wanakiri kuwepo kwa tatizo hili, na wameandaa mipango ya kuboresha kwa kiasi kikubwa sekta ya maji nchini Tanzania ifikapo mwaka 2015/2016. Hata hivyo, matokeo chanya ni madogo sana. Kama takwimu zetu zinavyoonesha katika kijarida hiki, upatikanaji wa maji ya bomba maeneo ya vijijini nchini Tanzania bado ni duni sana. Kuchota maji kumeendelea kuwa kazi inayochukua muda mwingi na kwa kiwango kikubwa hufanywa na wanawake. Idadi kubwa ya wananchi hawaoni mabadiliko yoyote katika sekta ya maji licha ya malengo makubwa yaliyowekwa na Mpango wa Matokeo Makubwa Sasa (BRN).

Licha ya hayo, Tanzania iko nyuma kwenye viwango vya kimataifa na kikanda. Kwa mujibu wa ripoti ya Shirika la Afya Duniani (WHO) na UNICEF ya mwaka 2014, Tanzania haikuwa na uwezekano wa kufikia lengo lake la MDG la kuongeza upatikanaji wa vyanzo bora vya maji ya kunywa ifikapo Desemba 2015[7]. Lengo hili tayari lilikuwa limefikiwa na nchi 116 mwaka 2012[8]. Nchi zingine 31 zilionekana kuwa kwenye hatua nzuri ya kufikia lengo hilo ifikapo mwishoni mwa mwaka 2015[9]. Tanzania imeshuka ukilinganisha na nchi za Kenya na Uganda katika kutoa huduma ya maji safi kwa wananchi wake. Upatikanaji wa maji safi kutoka vyanzo bora nchini Uganda (asilimia 75) tayari umeshafikia lengo la MDG, na Kenya ilionekana kukaribaia (asilimia 62). Kenya iliizidi Tanzania kwa asilimia 10 (Tanzania ilikuwa na asilimia 52) mwaka 2012. Kutokana na malengo mpya ya Malengo Mapya ya Maendeleo Endelevu ni kuhakikisha watu wote wanapata maji safi na salama, Tanzania itakuwa inaanzia chini zaidi kuliko nchi jirani, na itakuwa na kazi ngumu ya kufikia lengo hili kubwa.

Kwa kuwa serikali mpya inaanza kazi yake, ni fursa ya kipekee kufikiria upya mkakati wa maji wa Tanzania. Rais na mawaziri wake wanapaswa kutathmini mipango iliyopita ili kujua ni kwanini baadhi ya malengo yaliyowekwa hayakufikiwa, na iandaliwe mikakati mipya ya kuboresha upatikanaji wa maji hatua kwa hatua katika maeneo yote nchini, hasa maeneo ya vijijini. Licha ya ongezeko kubwa la bajeti kwenye sekta ya maji miaka ya hivi karibuni, asilimia ya watu wanaopata huduma ya maji imebaki ile ile na haijabadilika. Tanzania ikiwa na wakazi wengi waliotawanyika katika eneo kubwa la nchi, inakabiliwa na changamoto ya kipekee ya kuhakikisha watu wote wanapata maji safi. Ikumbukwe kuwa maji safi ya kunywa ni haki ya msingi na ni muhimu kwa afya bora, hasa kwa watoto wadogo. Hivyo, tunahitaji kufikiri kibunifu zaidi na kwa haraka jinsi ya kuhakikisha wananchi wote wanapata maji safi na salama pale walipo na usambaji maji unakuwa wa uhakika muda wote.

---

7 *Maendeleo juu ya Maji ya kunywa na Usafi: taarifa za hivi sasa 2014*. N.p.: n.p., n.d. tovuti ya WHO na UNICEF, 2014.

8 Ibid.

9 Ibid.